

القرآن الحكيم

QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

by
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy
(Former Chief Kadhi of
Zanzibar & Kenya)

57. Basi tulimwoko ya yeye na wafuasi wake ila mkewe, tukamkadiria katika wakao nyuma (wapate kuadhibiwa kwani alikuwa mtu mbaya kama hao).

58. Na tukawanyeshelezea, (tukawateremshia) mvua (ya mawe); na ilikuwa mbaya namna gani mvua ya wale walioonywa (wasisikie).

59. Sema: Sifa njema ni za Mwenyezi Mungu, na amani iwaendee watumwa wake aliowachagua. Je, Mwenyezi Mungu ni Bora au wale wanaowashirikisha (na Mwenyezi Mungu ndio bora)?

60. Au Yule aliyeziumba mbingu na ardhi, na akakuteremshieni maji kutoka mawinguni (siye bora?). Na kwa hayo tukaziotisha bustani zenye kupendeza, (mashamba yenye kupendeza). Nyinyi hamna uweza wa kuiotesha miti yake hii. Je, yuko Mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu? Bali hao (makafiri) ni watu wenye kwenda upogo, (kwenda upande).

61. Au Yule aliyefanya ardhi kuwa mahali pa matulio (yenu), na akaweka ndani yake mito na akaiwekea milima, na akaweka kizuizi baina ya bahari mbili, (bahari ya tamu na bahari ya chumvi, siye bora?). Je, yuko Mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Bali wengi katika wao hawajui (jambo, wanajifuatia ovyo ovyo tu).

62. Au Yule anayemjibu aliyedhikika amwombapo na kuondoa dhiki (yake) na kukufanyeni wenye kuendesha dunia (siye bora?). Je, yuko Mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Ni kuchache kuwaidhika kwenu.

63. Au Yule anayekuongozeni katika giza la bara na bahari, na azipelekaye pepo kuleta habari njema kabla ya rehema zake, (kabla ya kuja mvua, siye bora?). Je, yuko Mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Mwenyezi Mungu ametakasika na hao wanaowashirikisha naye.

64. Au Yule aliyeanzisha viumbe, kisha atavirudisha, na anayekuruzukuni kutoka mbinguni na kwenye ardhi, (siye bora?). Je, yuko Mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Sema: "Leteni dalili zenu ikiwa mnasema kweli (kuwa yuko mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu)."

فَأَنجَيْنَاهُ وَأَهْلَهُ إِلَّا امْرَأَتَهُ قَدَّرْنَاهَا مِنَ
الْعَابِرِينَ ۝

فَأَمْطَرْنَا عَلَيْهِمْ مَطَرًا فَسَاءَ مَطَرُ الْمُنْذَرِينَ ۝

قُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ وَسَلَامٌ عَلَى عِبَادِهِ الَّذِينَ
أَصْطَفَى ۚ اللَّهُ خَيْرٌ أَمَّا يُشْرِكُونَ ۝

أَمَّنْ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَأَنْزَلَ لَكُمْ
مِّنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَنْبَتْنَا بِهِ حَدَائِقَ ذَاتَ بَهْجَةٍ
مَا كَانَ لَكُمْ أَنْ تُنبِتُوا شَجَرَهَا ۚ إِنَّهُم مَّعَ اللَّهِ
هُمْ قَوْمٌ يَعِدُونَ ۝

أَمَّنْ جَعَلَ الْأَرْضَ قَرَارًا وَجَعَلَ خَلْقَهَا
أَنْهَارًا وَجَعَلَ لَهَا رَوَابِي وَجَعَلَ بَيْنَ الْبَحْرَيْنِ
حَاجِزًا ۚ إِنَّهُم مَّعَ اللَّهِ ۚ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ۝

أَمَّنْ يُجِيبُ الْمُضْطَرَّ إِذَا دَعَاهُ وَيَكْشِفُ السُّوءَ
وَيَجْعَلُ لَكُمْ خُلَفَاءَ ۚ إِنَّهُم مَّعَ اللَّهِ ۚ قَلِيلًا مَّا
تَذَكَّرُونَ ۝

أَمَّنْ يَهْدِيكُمْ فِي ظُلُمَاتِ الْبَرِّ وَالْبَحْرِ وَمَنْ
يُرْسِلُ الرِّيْحَ بُشْرًا بَيْنَ يَدَيْ رَحْمَتِهِ ۚ إِنَّهُم مَّعَ
اللَّهِ ۚ تَعَالَى اللَّهُ عَمَّا يُشْرِكُونَ ۝

أَمَّنْ يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ وَمَنْ يَنْزِعُكُمْ مِنَ السَّمَاءِ
وَالْأَرْضِ ۚ إِنَّهُم مَّعَ اللَّهِ ۚ قُلْ هَاتُوا بُرْهَانَكُمْ إِنْ
كُنْتُمْ صَادِقِينَ ۝

60-65. Zinatajwa baadhi ya sifa za Mwenyezi Mungu. Basi tumuachie Mwenyewe Mwenyezi Mungu aliye nazo khasa, siyo kuwapa walio makaburini na mizimu na . . . Kwa hawamiliki jambo katika haya.

65. Sema: "Hakuna aliyoko katika mbingu na ardhi ajuaye Ghayb (yasiyotokea) ila Mwenyezi Mungu; nao (hao wanaowaabudu) hawajui ni lini watafufuliwa, (watayajua mengineyo?)."

66. Kwani imewawivia lini ilimu yao (kuijua) akhera (hata wanauliza kitakuja lini hicho Kiama?). Bali wao wamo katika shaka nayo, bali wao ni vipofu nayo.

67. Na wale waliokufuru walisema: "Je, tutakapokuwa mchanga, (sisi) na baba zetu, (wazee wetu) ndio tutatolewa (makaburini mwetu, na hali ya kuwa tu hai tena?)."

68. "Bila shaka haya tuliahidiwa sisi na (wakaahidiwa) baba zetu zamani; hayakuwa haya ila ni visa (vya uwongo) vya watu wa kale."

69. Sema: "Nendeni katika ardhi na mwone jinsi ulivyokuwa mwisho wa wale wabaya."

70. Wala usiwahuzunikie, wala usiwe katika dhiki kwa sababu ya hila wanazozifanya.

71. Na wanasema, "Ahadi hii (ya kuja Kiama) itatokea lini, ikiwa mnasema kweli?"

72. Sema: "Asaa ni karibu kukufikieni sehemu ya yale mnayoyahimiza."

73. Na bila shaka Mola wako ni Mwenye fadhila kwa watu, lakini wengi wao hawashukuru.

74. Na kwa yakini Mola wako anayajua yanayoficha vifua vyao na wanayoyadhihirisha.

75. Na hakuna siri katika mbingu na ardhi ila imo katika kitabu (cha Mwenyezi Mungu) kibainishacho (kila kitu).

76. Bila shaka Qurani hii inawaeleza wana wa Israeli mengi ambayo kwayo wanahitilafiana.

77. Na kwa yakini hiyo (Qurani) ni uwongofu na rehema kwa wale wanaoamini.

78. Hakika Mola wako atawahukumu kwa hukumu yake (ya haki), naye ni Mwenye nguvu, Mjuzi.

79. Basi tawakali kwa Mwenyezi Mungu; hakika wewe uko juu (ya njia) ya haki iliyo wazi.

80. Kwa hakika huwezi kuwasikilizisha wafu mwito (wako) wala kuwasikilizisha viziwi, (hasa) wanapogeuka wanakwenda zao.

قُلْ لَا يَعْلَمُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ الْغَيْبَ إِلَّا اللَّهُ وَمَا يَشْعُرُونَ أَيَّانَ يُبْعَثُونَ ﴿٦٥﴾

بَلْ أَدْرَكَ عَلَيْهِمْ فِي الْآخِرَةِ بَلْ هُمْ فِي شَكٍّ مِنْهَا ۖ بَلْ هُمْ عَنْهَا مُعْمَوْنَ ﴿٦٦﴾

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا إِذَا كُنَّا تُرَابًا وَآبَاءُنَا أَيْسًا نُحْرَجُونَ ﴿٦٧﴾

كَفَرُوا بِهَذَا هَذَا نَحْنُ وَآبَاءُنَا مِنْ قَبْلُ ۖ إِنْ هَذَا إِلَّا أَسَاطِيرُ الْأَوَّلِينَ ﴿٦٨﴾

قُلْ سِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَانظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُجْرِمِينَ ﴿٦٩﴾

وَلَا تَحْزَنْ عَلَيْهِمْ وَلَا تَكُنْ فِي ضَيْقٍ مِمَّا يَمْكُرُونَ ﴿٧٠﴾

وَيَقُولُونَ مَتَى هَذَا الْوَعْدُ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٧١﴾

قُلْ عَسَى أَنْ يَكُونَ رَدْفٌ لَكُمْ بَعْضُ الَّذِي تَسْتَعْجِلُونَ ﴿٧٢﴾

وَأَنَّ رَبَّكَ لَذُو فَضْلٍ عَلَى النَّاسِ وَلَكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَشْكُرُونَ ﴿٧٣﴾

وَأَنَّ رَبَّكَ لَيَعْلَمُ مَا كُنْتُمْ صُدُّوهُمْ وَمَا يُعَلِّتُونَ ﴿٧٤﴾

وَمَا مِنْ عَائِدَةٍ فِي السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٧٥﴾

إِنَّ هَذَا الْقُرْآنَ يَفُصِّلُ عَلَى نَبِيِّ إِسْرَائِيلَ أَكْثَرَ الَّذِي هُمْ فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿٧٦﴾

وَأَنَّهُ لَهْدَى وَرَحْمَةً لِّلْمُؤْمِنِينَ ﴿٧٧﴾

إِنَّ رَبَّكَ يَقْضِي بَيْنَهُمْ بِحُكْمِهِ ۖ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْعَلِيمُ ﴿٧٨﴾

فَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ إِنَّكَ عَلَى الْحَقِّ الْمُبِينِ ﴿٧٩﴾

إِنَّكَ لَا تَسْمِعُ الْمَوْتَى وَلَا تَسْمِعُ الصُّمَّ الدُّعَاءَ إِذَا وَلُوا مَدْبِرِينَ ﴿٨٠﴾

81. Wala huwezi kuwaongoza vipofu katika upotofu wao. Huwezi kuwasikilizisha isipokuwa wale wanaoziamini Aya zetu, basi hao ndio watii.

82. Na kauli (ya kuja Kiama) itakapowathibitikia tutawatolea mnyama katika ardhi atakayewasemeza kwa sababu watu walikuwa hawaziyakinishi Aya zetu.

83. Na (wakumbushe) siku tutakapokusanya katika kila uma makundi ya wale wanaokadhibisha Aya zetu, nao watawekwa mafungu mafungu.

84. Hata watakapofika, atasema (Mwenyezi Mungu kuwaambia): "Je, nyinyi mlizikadhibisha Aya zangu pasipo kuzijua (kwanza) vyema? (Mlikadhibisha bila ya kufikiri kwanza) Au mlikuwa mkifanya nini?"

85. Na itawathibitikia kauli (ya kuadhibiwa) kwa sababu ya (kule) kudhulumu (kwao nafsi zao). Basi hawatasema (lo lote). (Angurumapo Simba husema nani?).

86. Je, hawaoni ya kwamba tumeuumba usiku (makusudi) ili watulie humo, (wapumuwe), na mchana uwangazao (ili waone)? Kwa yakini katika hayo zimo alama (kubwa) kwa watu wanaoamini. (Wakaona rehema za Mwenyezi Mungu zilizo juu ya viumbe vyake).

87. Na (wakumbushe) siku litakapopulizwa parapanda, (baragumu la Kiama); wahangaika waliomo mbinguni na waliomo ardhini ila yule ambaye Mwenyezi Mungu (anataka asihangaika), (asifazaike); na wote watamfikia (Mwenyezi Mungu), hali ya kuwa wadhalilifu.

88. Na unaiona milima unaidhania imetulia; nayo inakwenda kama mawingu (yanavyokwenda). Ndiyo sanaa ya Mwenyezi Mungu, (matengenezo yake) aliyekitengeneza kila kitu; bila shaka anazo habari za yote mnayoyatenda.

وَمَا أَنْتَ بِهَادِي الْعَمَىٰ عَنْ ضَلَالَتِهِمْ إِنْ نَسِيتُ إِلَّا
مَنْ يُّؤْمِنُ بِآيَاتِنَا فَهُمْ مُّسْلِمُونَ ﴿٨١﴾

وَإِذَا وَقَعَ الْقَوْلُ عَلَيْهِمْ أَخْرَجْنَا لَهُمْ دَابَّةً مِّنَ
الْأَرْضِ تُكَلِّمُهُمْ أَنَّ النَّاسَ كَانُوا بِآيَاتِنَا لَا يُوقِنُونَ ﴿٨٢﴾

وَيَوْمَ نَحْشُرُ مِنْ كُلِّ أُمَّةٍ فَوْجًا مِّمَّنْ يُكَذِّبُ بِآيَاتِنَا
فَهُمْ يُفْرَعُونَ ﴿٨٣﴾

كَذَّبُوا إِذَا جَاءَ وَقَالَ أَكْذَبْتُمْ بآيَاتِي وَلَمْ تُحِيطُوا بِهَا
عَلَمًا أَمَا ذَاكُنْتُمْ تُفْعَلُونَ ﴿٨٤﴾

وَوَقَعَ الْقَوْلُ عَلَيْهِمْ بِمَا ظَلَمُوا فَهُمْ لَا يَنْطِقُونَ ﴿٨٥﴾

الْعَبِيرُوا أَنَّا جَعَلْنَا اللَّيْلَ لَيْسَكُنَّ فِيهِ وَالنَّهَارَ
مُبْصِرًا إِنْ فِي ذَلِكَ لَايَاتٍ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٨٦﴾

وَيَوْمَ يُنْفَخُ فِي الصُّورِ فَفَرَّقَ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَمَنْ
فِي الْأَرْضِ إِلَّا مَنْ شَاءَ اللَّهُ ۚ وَكُلٌّ أَتَوْهُ
ذُخْرَيْنَ ﴿٨٧﴾

وَتَرَى الْجِبَالَ تَحْسَبُهَا جَاوِدَةً وَهِيَ تَمُرُّ مَرَّ السَّحَابِ
صُمِعَ لِلَّهِ الَّذِي أَنْشَأَ كُلَّ شَيْءٍ إِنَّهُ خَبِيرٌ بِمَا
تَفْعَلُونَ ﴿٨٨﴾

82. Haya mambo ya Kiakhhera; tusitafute kuyajua hakika yake tangu hapa leo. Hakika yake itajulikana huko. Hapa ni kuamini tu.

Makadiyani wamepachika hapa uwongo wao wa kusema: "Masihi aliyeahidiwa."

Uwongo mtupu kama tulivyobainisha haya katika Aya ya 115 ya *Suratul Baqarah*.

88. Na hili vile vile katika hayo yaliyosemwa katika Qurahi myaka 1400 leo. Na ndiyo kwanza sasa maulamaa wa huko Ulaya wametambua haya: kuwa Dunia Inazunguka.

Makadiyani wametia hapa kwenye hii Aya waliyoifanya kuwa ya 89 tafsiri yao ya uwongo ya kufasiri "*Al Jibal*." Tumebainisha uwongo wao huu katika marejezo ya Aya ya 105 ya *Surat Taha*. Basi yote hayo waliyoyatia ni tarumu tupu — hayakhusu ndewe wala sikio.

89. Watakaoleta mema, watapata mema kuliko hayo nao mahangaiko ya siku hiyo watasalimika nayo.

90. Na watakaolera ubaya, basi zitasunukishwa nyuso zao Motoni (waambiwe): "Kwani mnalipwa (kwa mengine) isipokuwa yale mliyokuwa mkiyatenda?"

91. Bila shaka nimeamrisha nimwabudu Mola wa mji huu (wa Makka) ambaye ameutukuza; na ni vyake tu (Mwenyezi Mungu) vitu vyote na nimeamrisha niwe miongoni mwa wanaonyenyekea:

92. Na (nimeamrisha) nisome Qurani. Na mwenye kuongoka, ameongoka kwa (faida ya) nafsi yake; na aliyepotea (anapotea kwa madhara ya nafsi yake). Sema: "Hakika mimi ni miongoni mwa Waonyaji, (Mitume; sina zaidi kuliko hili)."

93. Na sema: "Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu. ("Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu"), karibuni hivi atakuonyesheni Ishara zake na mtazifahamu;" wala Mola wako haghafiliki na hayo mnayofanya.

مَنْ جَاءَ بِالْحَسَنَةِ فَلَهُ خَيْرٌ مِنْهَا، وَهُمْ مِّنْ فَتْرَةٍ
يَوْمَئِذٍ أَعْمُونَ ﴿٨٩﴾


وَمَنْ جَاءَ بِالسَّيِّئَةِ فَكُبَّتْ وُجُوهُهُمْ فِي النَّارِ هَلْ
يُخْرَجُونَ إِلَّا مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٩٠﴾

إِنَّمَا أَمَرْتُ أَنْ أَعْبُدَ رَبَّ هَذِهِ الْبَلَدَةِ الَّذِي
حَرَّمَهَا وَلَهُ كُلُّ شَيْءٍ وَإِنَّمَا أَمَرْتُ أَنْ أَكُونَ مِنَ
الْمُسْلِمِينَ ﴿٩١﴾

وَأَنْ أَتْلُو الْقُرْآنَ، فَمَنِ اهْتَدَىٰ فَإِنَّمَا يَهْتَدِي لِنَفْسِهِ
وَمَنْ ضَلَّ فَقُلْ إِنَّمَا أَنَا مِنَ الْمُنذِرِينَ ﴿٩٢﴾

وَقُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ سَيَرْيَكُم أَيْتَهُ فَتَعْرِفُونَهَا، وَمَا رَبُّكَ
بِغَافِلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٩٣﴾

92. Watu wanahimizwa kusoma Qurani kila wakati kama ilivyo hapa; na katika kila jambo, kama ilivyo katika Aya ya 61 ya Surat Yunus; na wanasifiwa wanaosoma Qurani, kama ilivyo katika Aya ya 29 ya Surat Fatir na nyinginezo; wakahadidiwa wanaopuuza kama ilivyo katika Aya ya 100 ya Surat Taha na nyinginezo; na Mtume akapiga kelele kuwa watu wanaitupa Qurani kama ilivyo katika Aya ya 30 ya Suratul Furqan. Na juu ya hivi baadhi ya Waislamu wanaipuuza na kushughulikia Manyiradi bali Makasida. Isiwe hivi



Inu Aya 88

SURATUL QASAS

Inu Makuru 9

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Taa Syn Mym.
2. Hizi ni Aya za Kitabu kinachobainisha (kila kinachohitajiwa katika dini).
3. Tunakusomea habari za Musa na Firauni kwa (njia ya) haki kwa ajili ya watu wanaoamini.

طسّم ١

تِلْكَ آيَاتُ الْكِتَابِ الْمُبِينِ ١

4. Hakika . Firauni alitakabari (alijitukuza) katika ardhi, na akawafanya watu wa huko makundi mbali mbali. Akalidhoofisha kundi moja miongoni mwao, akiwachinja watoto wao wanaume na kuwawacha hai watoto wao wanawake. Hakika yeye alikuwa miongoni mwa waharibifu (kabisa).

نَتْلُو عَلَيْكَ مِنْ نَبَأِ مُوسَى وَفِرْعَوْنَ بِالْحَقِّ لِقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ٢

5. Na tukataka kuwafanyia ihsani wale waliodhoofishwa katika ardhi hiyo na kuwafanya viongozi, na kuwafanya warithi (wa neema hizo).

إِنَّ فِرْعَوْنَ عَلَا فِي الْأَرْضِ وَجَعَلَ أَهْلَهَا شِيْعًا يَبْتَعْضِفُ طَائِفَةً مِنْهُمْ يُدَبِّرِ الْأَمْرَ وَتَتَّبِعِي نِسَاءَهُمْ إِنَّهُ كَانَ مِنَ الْمُفْسِدِينَ ٣

6. Na kuwapa nguvu ardhini; na kumwonyesha Firauni na Hamana na majeshi yao, yale waliyokuwa wakiyaogopa.

وَنُرِيدُ أَنْ نَمُنَّ عَلَى الَّذِينَ اسْتُضِعُوا فِي الْأَرْضِ وَنَجْعَلَهُمْ أَئِمَّةً وَنَجْعَلَهُمُ الْوَارِثِينَ ٤

7. Tulimfunulia mama yake Musa (tuliutia fahamu moyo wake) ya kwamba mnyonyeshe, na utakapomhofia, basi mtie mtoni, na usiogope wala usihuzunike, kwani sisi tutamrudisha kwako, na tutamfanya miongoni mwa Mitume.

وَنُكَلِّبُ لَهُمْ فِي الْأَرْضِ وَنُرِي فِرْعَوْنَ وَهَامَانَ وَجُنُودَهُمَا مِنْهُمْ مَا كَانُوا يَحْذَرُونَ ٥

8. Basi wakamwokota watu wa Firauni. Ili awe adui kwao na huzuni; bila shaka Firauni na Hamana na majeshi yao walikuwa wenye uwovu.

وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ أُمِّ مُوسَىٰ أَنْ أَرْضِعِيهِ ۖ فَإِذَا خَفَتْ عَلَيْهِ قَالِقِيهِ فِي الْبَيْتِ وَلَا تَخَافِي وَلَا تَحْزَنِي ۚ إِنَّا رَأَيْنَاهُ إِلَيْكَ وَجَاءَ عِلْوَهُ مِنَ الْمُرْسَلِينَ ٦

9. Na mkewe Firauni (alipomwokota yule mtoto) alisema (kumwambia Firauni alipoamrisha auwawe yule mtoto; alimwambia "Usimwue, atakuwa kiburudisho cha macho kwangu na kwako; na msimwue, huenda atatunufaisha, au tumpange kuwa mtoto (wetu)." (Walisema haya na) hali hawatambui (kuwa atakuwa adui yao).

فَالْقَطْعُ ۚ أَلْ فِرْعَوْنَ لِيَكُونَ لَهُمْ عَدُوًّا وَحَزَنًا ۚ إِنَّ فِرْعَوْنَ وَ هَامَانَ وَجُنُودَهُمَا كَانُوا خَاطِبِينَ ٧

وَقَالَتِ امْرَأَتُ فِرْعَوْنَ قُرْتُ عَيْنِي لِي وَلَكَ ۚ لَا تَقْتُلُوهُ ۚ عَسَىٰ أَنْ يَنْفَعَنَا أَوْ نَتَّخِذَهُ وَلَدًا وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ٨

10. Na moyo wa mama yake Musa ukawa mtupu, (hauna fikira ila ya mwanawe tu); alikuwa karibu kudhihirisha (siri ile ya kuwa yule ni mtoto wake) kama tusingeutia nguvu moyo wake ili awe miongoni mwa wenye kuamini (ahadi ya Mwenyezi Mungu).

11. Na (huyo mama yake Musa) akamwambia dada yake (Musa): "Mfuata." (Fuata njia anayochukuliwa na maji). Basi yeye akamwalia kwa mbali bila wao kujua

12. Na tukamuharimishia wanyonyeshaji tangu mwanzo. Na (dada yake) akasema: "Je, nikuonyesheni watu wa nyumba watakawomlea kwa ajili yenu, na pia watakuwa mwema kwake?" (Wakakubali: Basi akawatajia mama yake ambaye ndiye mama yake Nabii Musa).

13. Basi tukamrudisha kwa mama yake ili macho yake yaburudike, (moyo wake utuwe), wala asihuzunike; na ajue ya kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli, lakini wengi wao hawajui.

14. Na (Musa) alipofikia balebhe yake na akastawi, tulimpa akili na ilimu; na hivi ndivyo tuwalipavyo wafanyao mema.

15. Akaingia mjini (siku moja) wakati wenyeji wake walikuwa katika ghafla, (yaani katikati ya mchana), na akakuta humo watu wawili wakipigana: mmoja ni katika jamaa zake na mwengine katika adui zake (Adui za Mayahudi). Basi yule jamaa yake alimwomba msaada juu ya yule adui yake. Musa akampiga ngumi, akammaliza, (akafa hapo hapo). Akasema, "Hiki (nilichokifanya) ni kitendo cha Shetani; bila shaka yeye ni adui, mpotezaji dhahiri!"

16. Akasema: "Mola wangu! Bila shaka nimedhulumu nafsi yangu, basi nisamehe;" Naye (Mwenyezi Mungu) akamsamehe (kwani hakufanya kusudi). Kwa yakini Yeye ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

17. Akasema: "Mola wangu! Kwa kuwa umenineemesha, basi sitakuwa kabisa msaidizi wa watu wabaya."

18. Akapambazukiwa mjini asubuhi (siku ya pili yake), naye ana khofu, anangoja (lipi litamfika kwa yale yaliotokea jana); mara mtu yule aliyeomba msaada kwake jana, anamwita (amsaidie kupigana na adui yake mwengine); Musa akamwambia: "Bila

وَأَصْبَحَ فُؤَادُ أَرْمُوسَىٰ فِرْعَاوْنَ كَاَدَتْ كَثْبِي يَوْمَ
لَوْلَا أَن رَّبَّنَا عَلَّ قَلْبَهَا لَشَكَّوْنَ مِنَ
الْمُؤْمِنِينَ ⑩

وَقَالَتْ لِأُخْتِهِ قُصِّيهِ، فَبَصُرَتْ بِهِ عَنْ جُنْبٍ
وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ⑪

وَحَرَّمْنَا عَلَيْهِ الْمَرَاضِعَ مِنْ قَبْلُ فَقَالَتْ هَلْ
أَدْرُكُمْ عَلَىٰ أَهْلِ بَيْتٍ يَكْفُلُونَهُ لَكُمْ وَهُمْ لَهُ
نَصْحُونَ ⑫

فَرَدَدْنَاهُ إِلَىٰ آوِيهِ كَيْ تَقَرَّ عَيْنُهَا وَلَا تَحْزَنَ
وَلَنَعْلَمَ أَنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ وَلَكِنْ أَكْثَرُهُمْ لَا
يَعْلَمُونَ ⑬

وَلَمَّا بَلَغَ أَشُدَّهُ وَاسْتَوَىٰ آتَيْنَاهُ حُكْمًا وَعِلْمًا
وَكَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ⑭

وَدَخَلَ الْمَدِينَةَ عَلَىٰ حِينٍ غَفْلَةٍ مِّنْ أَهْلِهَا
فَوَجَدَ فِيهَا رَجُلَيْنِ يَقْتَتِلَانِ هَٰذَا مِنْ شِيعَةِ
وَهَٰذَا مِنْ عَدُوِّهِ فَاسْتَغَاثَهُ الَّذِي مِّنْ شِيعَتِهِ عَلَى
الَّذِي مِّنْ عَدُوِّهِ فَزَكَرَهُ مُوسَىٰ فَقَضَىٰ عَلَيْهِ، قَالَ
هَٰذَا مِنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ إِنَّهُ عَدُوٌّ مُّضِلٌّ مُّبِينٌ ⑮

قَالَ رَبِّ إِنِّي ظَلَمْتُ نَفْسِي فَاغْفِرْ لِي فَغَفَرَ لَهُ
إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ⑯

قَالَ رَبِّ إِنَّمَا اتَّخَفْتُ عَلَىٰ فُلْنٍ لَّا أَكُونُ ظَاهِرًا
لِّلْمُجْرِمِينَ ⑰

فَأَصْبَحَ فِي الْمَدِينَةِ خَائِفًا يَتَرَقَّبُ فَإِذَا الَّذِي
اسْتَصْرَفَهُ بِالْأَمْسِ يَسْتَصْرِفُهُ قَالَ لَهُ مُوسَىٰ

shaka wewe ni mpotofu uliye dhahiri; (kila siku hwishi ugomvi?).”

19. Basi alipotaka kumtia mkononi yule aliye adui yao wote wawili, (yule mwenye kutaka msaada alidhani kuwa Nabii Musa anataka kumpiga yeye) akasema: “Ewe Musa!. Unataka kuniua kama ulivyomwua mtu jana? Wewe hutaki ila kuwa jabari katika nchi wala hutaki kuwa miongoni mwa watu wazuri. (Basi ikatangaa habari hii kuwa Musa ndiye aliyemwua yule mtu jana).”

20. (Firauni akaamrisha akamatwe Musa po pote atakapoonekana). Basi akaja mtu kutoka mwisho wa mji akipiga mbio, akasema: “Ewe Musa! Wakubwa wanashauriana kukuua, basi ondoka (katika nchi hii); bila shaka mimi ni miongoni mwa wakutakiao mema.”

21. Basi (Musa) akatoka, na huku anaogopa, anangoja (lipi litamfika, na) akasema: “Mola wangu, niokoe na watu madhalimu.”

22. Na alipoelekea upande wa Madiani, (nchi katika Bara Arabu) alisema “Asaa Mola wangu ataniongoza njia iliyo sawa.”

23. Na alipoyafikia maji ya Madiani, (mahali wanapoteka maji watu wa hapo) alikuta kundi la watu wananywesha (wanyama wao), na akakuta kando yao wanawake wawili wanazuia (wanyama wao wasende kunywa maji pamoja na wale wanyama wengine). Akasema (Musa): “Mna nini? (Mbona hamteki na nyinyi na kunywesha wanyama wenu?)” Wote wawili wakasema: “Hatunyweshi mpaka wachungaji warudishe (wanyama wao; hatuwezi kupigana nao vikumbo), na baba yetu ni mzee sana.”

24. Basi (Musa) akawanyweshea, kisha akarudi kivulini, na akasema: “Mola wangu! Bila shaka mimi ni mhitaji wa heri utakayoniteremshia.”

25. Basi akamjia mmoja katika wale wawili, anakwenda na huku anaona haya, akasema: “Baba yangu anakuita ili akulipe ujira wa kutunyweshea.” Basi alipomfikia na akamsimulia kisa chote, alisema: “Usiogope umekwisha kuokoka na watu madhalimu.”

26. Akasema mmoja wa wale wawili: “Ewe baba yangu! Mkodi huyu (awe anachunga wanyama

إِنَّكَ لَتَعُولِي مُبِينٌ ۝

فَلَمَّا أَنْ أَرَادَ أَنْ يَنْبَاشَ بِالَّذِي هُوَعَدُ لَهُمَا، قَالَ يَمُوسَى أَتُرِيدُ أَنْ تَقْتُلَنِي كَمَا قَتَلْتَ نَفْسًا بِالْأَمْسِ إِمَّا تُرِيدُ إِلَّا أَنْ تَكُونَ جَبَّارًا فِي الْأَرْضِ وَمَا تُرِيدُ أَنْ تَكُونَ مِنَ الْمَصْلُحِينَ ۝

وَجَاءَ رَجُلٌ مِنْ أَقْصَا الْمَدْيَنَةِ يَسْعَى، قَالَ يَمُوسَى إِنَّ الْمَلَائِكَةَ يَأْتِيهِمْ بِكَ لِيَقْتُلُوكَ فَاحْذَرِ إِنِّي لَكَ مِنَ النَّاصِحِينَ ۝

فَحَذَرَهَا خَائِفًا يَتَرَقَّبُ قَالَ رَبِّ نَجِّنِي مِنَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ۝

وَلَمَّا تَوَجَّهَ تَلَقَّاهُ مَدْيَنَ قَالَ عَلَى لَيْقَى أَنْ يَهْدِيَنِي سَوَاءَ السَّبِيلِ ۝

وَلَمَّا وَرَدَ مَاءَ مَدْيَنَ وَجَدَ عَلَيْهِ أُمَّةٌ مِنَ النَّاسِ يَسْقُونَ هُوَ وَجَدَ مِنْ دُونِهِمْ امْرَأَتَيْنِ تَذُودَانِ قَالَ مَاطْطَبَكُمَا قَالَتَا لَا نَسْقِي حَتَّى يُصْدِيَ الْإِعَادُ ۝

فَسَقَى لَهُمَا ثُمَّ تَوَلَّى إِلَى الظِّلِّ فَقَالَ رَبِّ إِنِّي لِمَا أَنْزَلْتَ إِلَيَّ مِنْ خَيْرٍ فَقِيرٌ ۝

فَجَاءَتْهُ إِحْدَاهُمَا تَتَشَّى عَلَى الشَّجَرِ قَالَتْ إِنَّ أَبِي يَدْعُوكَ لِيَجْزِيَكَ أَجْرَ مَا سَقَيْتَ لَنَا، فَلَمَّا جَاءَهُ وَقَصَّ عَلَيْهِ الْقَصَصَ قَالَ لَا تَخَفْ نَجَوْتَ مِنَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ۝

قَالَتْ إِحْدَاهُمَا يَا أَبَتِ اسْتَأْجِرْهُ إِنَّ خَيْرَ مَنِ

26. Hapa huyu mtoto mwanamke katoa rai kumpa baba yake. Na baba yake alipoiona ni rai razuri aliikubali akaifuata. Na Mtume alifuata rai za wanawake vile vile alipoona ni rai za kufuatwa, kama rai za Bibi Khadija fangu

wako badili yetu). Bila shaka mbora uwezaye kumwajiri ni ambaye mwenye nguvu, mwaminifu (Na huyu ana sifa zote hizo)."

27. Akasema: "Mimi nataka nikuoze mmojawapo katika binti zangu hawa wawili kwa kunitumikia miaka minane; na kama ukitimiza kumi ni hiari yako, lakini mimi sitaki kukutaabisha: utanikuta Insha-Allah miongoni mwa watu wema."

28. Akasema (Musa: "Mapatano) hayo yamekwisha kuwa baina yangu na baina yako; muda mmojapo nitakaoumaliza, basi nisidhulumiwe; na Mwenyezi Mungu ni Mlinzi juu ya haya tunayoyasema."

29. Basi Musa alipotimiza muda, akasafiri pamoja na ahali zake (watu wake) (kurejea kwa Misri), aliona moto upande wa mlimani akawaambia ahali zake; "Ngojeni, hakika nimeona moto; labda nitakuleteeni habari za huko au kijinga cha moto ili muote."

30. Basi alipoufikia aliitwa kutoka upande wa kuliani wa bonde hilo, katika kiwanja kilichobarikiwa, kutoka mtini, "Ewe Musa! Bila shaka mimi ndiye Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu;"

31. "Na, tupa fimbo yako." Basi alipoiona ikicheza-cheza kama nyoka aligeuka kwenda zake wala hatazami nyuma, (akaambiewa) "Ewe Musa! Njoo mbele na usiogope, kwa yakini wewe ni miongoni mwa waliosalimika."

32. "Ingiza mkono wako kwenye mfuko wako (lisani ya kanzu yako) utatoka mweupe pasipo ubaya, na jiambatishie mkono wako ukihisi khofu; (ukifanya hivyo itaondoka)! Basi hizi zitakuwa dalili mbili zitokazo kwa Mola wako kwa ajili ya Firauni na wakuu (wa uma) wake; bila shaka hao ni watu maasi."

33. (Musa) akasema: "Mola wangu! Hakika mimi nilimwua mtu katika wao kwa hivyo naogopa wataniua."

اسْتَأْجَرَتِ الْقَوِيُّ الْأَيُّمِينَ ①

قَالَ إِنِّي أُرِيدُ أَنْ أَمْكِكَ بِحَدَى ابْنَتَيْنِ هَتَيْنِ عَلَى أَنْ تَأْجُرَنِي ثَمْنِي حَجْجٌ ۖ فَإِنْ أَنْسَمْتَ عَشْرًا فَمِنْ عِنْدِكَ ۚ وَمَا أُرِيدُ أَنْ أَمْكِكَ ۚ أَشَقُّ عَلَيْكَ مَسْعِدُنِي إِنْ شَاءَ اللَّهُ مِنَ الضَّلِيلِينَ ②

قَالَ ذَلِكَ بَيْنِي وَبَيْنَكَ أَيَّمَا الْأَجَلَيْنِ قَضَيْتُ ۖ فَلَا عُدْوَانَ عَلَيَّ وَاللَّهُ عَلَى مَا نَقُولُ وَكِيلٌ ③

فَلَمَّا قَضَى مُوسَى الْأَجَلَ وَسَارَ بِأَهْلِهِ آنَسَ مِنْ جَانِبِ الطُّورِ نَارًا ۚ قَالَ لِأَهْلِهِ امْكُثُوا إِنِّي آنَسْتُ نَارًا أَلْعَلِّي آتِيكُمْ مِنْهَا بِخَبَرٍ أَوْ جَذْوَةٍ مِنَ النَّارِ لَعَلَّكُمْ تَصْطَلُونَ ④

فَلَمَّا أَنهَا تُودِي مِنَ شَاطِئِ الْوَادِ الْأَيْمَنِ فِي الْبُقْعَةِ الْمُبْرَكَةِ مِنَ الشَّجَرَةِ أَنْ يُمُوسَى إِنِّي أَنَا اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ⑤

وَأَنْ أَلْقِ عَصَاكَ فَلَمَّا رَآهَا تُهَلِكُ كَانَتْهَا جَانٌّ وَكَلِّ مُدْبِرًا وَلَمْ يُعَقِّبْ ۚ يَمُوسَى أَقْبَلُ وَلَا تَخَفْ ۚ إِنَّكَ مِنَ الْآمِنِينَ ⑥

أَسْلَكَ يَدَكَ فِي جَيْبِكَ تَخْوَفَ بَيْضَاءَ مِنْ غَيْرِ سُوءٍ ۚ وَأَصْمَمَ إِلَيْكَ جَنَاحَكَ مِنَ الرَّهْبِ ۚ فَذَكَرَ بُرْهَانٍ مِنْ رَبِّكَ إِلَى فِرْعَوْنَ وَ مَلَائِكِهِ مِنْهُمْ كَانُوا قَوْمًا فَسِيقِينَ ⑦

قَالَ رَبِّ إِنِّي قَتَلْتُ مِنْهُمْ نَفْسًا فَأَخَافُ أَنْ يَقْتُلُونِ ⑧

siku ya mwanzo ya kuja Utume, na akafuata rai ya Bibi Khawla bint Hakym katika kumpendesha kumwoa Bibi Aisha na Bibi Sauda. na akafuata rai ya Bibi Ummu Salama katika umra ya *Sulhul Hundaybiya* na akafuata rai za wengine pia. Na juu ya hivi kuna Waislamu wanaosema kuwa Mtume amekataza kufuata rai za wanawake, na wakitoa rai zao zifanywe kinyume cha walivyosema. Na wanayatajia Hadithi maneno yao haya. Nayo ni *Shaawiruhunna Wakhaalifuuhunna*. Basi hii si Hadithi ya Mtume, kama ilivyo katika sahifa 88 ya kitabu cha kubainisha Hadithi sahihi na zisizokuwa sahihi kinachoitwa *Tamyizut Tayyib Minal Khabyih*, cha Sh. Addaybai, na vile vile katika kitabu cha *Al Maqaasidul Hasanah* cha Sh. As Sakhawy.

34. “Na ndugu yangu Haruni ni fasihi zaidi kuliko mimi kwa usemi, basi mtume pamoja nami awe msaidizi, kunisadikisha; hakika mimi naogopa ya kwamba watanikadhibisha.”

35. (Mwenyezi Mungu) akasema: “Tutautia nguvu mkono wako kwa ndugu yako, na tutakupeni ushindi hata hawatakufikieni. Kwa sababu ya ishara zetu nyinyi na watakaokufuateni mtashinda.”

36. Basi alipowajia Musa na hoja zetu waziwazi, walisema: “Hayakuwa haya ila ni uchawi uliotungwa, (kiini macho), wala hatukuyasikia haya kwa wazee wetu wa kale.”

37. Na Musa akasema: “Mola wangu anamjua yule ajaye na uwongofu kutoka Kwake, na yule atakayekuwa na mwisho (mzuri) wa makazi (mema); hakika madhalimu hawatafaulu.”

38. Na Firauni akasema: “Enyi wakuu! Simjui kwa ajili yenu mungu asiyekuwa mimi. Basi ewe Hamana! (Nifanyie matufali). Niwashie moto juu ya udongo (wa matufali hayo mpaka yakauke barabara) unijengee mnara ili nimchungulie Mungu wa Musa, na mimi namdhani kuwa yu katika waongo (lakini haidhuru, natwende nikamtazame huyo Mungu wake).”

39. Na alijivuna yeye na majeshi yake katika nchi pasi na haki na walidhani ya kwamba hawatarudishwa (hawatarejeshwa) kwetu.

40. Basi tukamtesha (tukamtesa) yeye na majeshi yake na tukawatupa (tukawatumbukiza) baharini, basi angalia ulikuwaje mwisho wa madhalimu.

41. Na tuliwafanya waongozi waitao katika Moto, na siku ya Kiama hawatanusuriwa.

42. Na tukawafuatishia laana katika dunia hii, na siku ya Kiama watakuwa miongoni mwa wenye hali mbaya (kabisa).

43. Na bila shaka tulimpa Musa kitabu baada ya kuziangamiza uma za kwanza (zilizopita); kiwe kifumbua macho cha watu (kiwaangazie) na kiwe uwongofu na rehema, ili wapate kukumbuka.

44. Wala wewe hukuwa upande wa magharibi (wa hilo jabali) Tulipompelekea Musa amri wala hukuwa miongoni mwa waliohudhuria (hapo)

45. Lakini sisi tuliumba uma nyingi (baada ya Nabii Musa hata ukaja wewe), na umri ukawa mrefu

وَإِنِّي هَارُونَ هُوَ أَفْضَحُ مِنِّي لِسَانًا فَأَرْسَلَهُ مَعِيَ رِدْءًا يُصَدِّقُنِي إِنِّي أَخَافُ أَنْ يُكَذِّبُونِ ۝

قَالَ سَنَشُدُّ عَضُدَكَ بِأَخِيكَ وَنَجْعَلُ لَكُمَا سُلْطٰنًا فَلَا يَصِلُونَ إِلَيْكُمَا بِآيَاتِنَا أَنْتُمَا وَمِنَ اتَّبَعَكُمَا الْغٰلِبُونَ ۝

فَلَمَّا جَاءَهُمْ مُوسَى بِآيَاتِنَا بَيِّنٰتٍ قَالُوا مَا هٰذَا إِلَّا سِحْرٌ مُّفْتَرًى وَمَا سَمِعْنَا بِهٰذَا فِي آبَائِنَا الْأَوَّلِينَ ۝

وَقَالَ مُوسَى رَبِّيْٓ أَعْلَمُ بِمَا يَفْعَلُ بِالْهٰدِيْنَ وَمَنْ عِنْدَهُ مَن يَكُونُ لَهُ عَاقِبَةُ الدَّارِ اِيْنَاهُ لَا يَفْلِحُ الظَّٰلِمُونَ ۝

وَقَالَ فِرْعَوْنُ يٰٓأَيُّهَا الْمَلٰٓئِكَةُ عَلِمْتُ لَكُمْ مِّنْ اِلٰهِ غَيْرِىْ ۚ فَآوَدْتُ لِىْٓ اِيْهَا مَنْ عَلَى الْاَرْضِ فَاجْعَلْ لِىْ صَرْحًا لَّعَلِّيْ اُظَلِّعُ اِلٰى اِلٰهِ مُوسٰى ۚ وَارِىْ لَظَنَّةً مِّنَ الْكَٰذِبِيْنَ ۝

وَاسْتَكَبَرَ هُوَ وَجُنُودُهُ فِي الْاَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَظَنُوْٓا اَنْهُمْ اِلٰٓئِهًا لَا يُرْجَعُوْنَ ۝

فَاَحْدَنَهُ وَجُودُهُ قَبْضَتُهُمْ فِيْ اَيْمٍ فَانْظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الظَّٰلِمِيْنَ ۝

وَجَعَلْنٰهُمْ اٰیَةً يُّدْعَوْنَ اِلَى النَّارِ وَيَوْمَ الْقِيٰمَةِ لَا يُنْصَرُوْنَ ۝

وَاتَّبَعْنٰهُمْ فِيْ هٰذِهِ الدُّنْيَا لَعْنَةً ۚ وَيَوْمَ الْقِيٰمَةِ هُمْ مِّنَ الْمَقْبُوْحِيْنَ ۝

وَلَقَدْ اٰتَيْنَا مُوسٰى الْكِتٰبَ مِنْۢ بَعْدِ مَا اَهْلَكْنَا الْقُرُوْنَ الْاَوَّلٰى بِصَٰرٍ لِّلنَّاسِ وَهٰدًى وَرَحْمَةً لَّعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُوْنَ ۝

وَمَا كُنْتَ بِجَانِبِ الْعَرَبِ اِذْ قَضَيْنَا اِلٰى مُوسٰى الْاَمْرَ وَمَا كُنْتَ مِنَ الشَّٰهِدِيْنَ ۝

وَتَكِيْكَ اَنْشَاْنَا قُرُوْٓنًا تَقٰوَلْ عَلَيْهِمُ الْعُمُرُ

juu yao, wala hukuwa mkazi na watu wa Madiana, unasoma kwao Aya zetu, lakini sisi Tulikuwa tunapeleka (Mitume na tunawapa habari za mambo yanayokuja na yaliyopita kama tulivyokupa wewe ukajua haya).

46. Wala hukuwa upande wa mlima tulipo mnadia (Nabii Musa), lakini (kutumwa kwako) ni rehema ya Mola wako, ili uwaonye watu wasiojiwa na muonyaji (kwa muda mrefu) kabla yako, hwenda watakumbuka.

47. (Wala tusingekuleta) ila isije ukawafikia msiba kwa yale iliyoyatanguliza mikono yao, wakasema: "Mola wetu! Mbona hukutuletea Mtume nasi, tukafuata Aya zako na tukawa miongoni mwa walioamini?"

48. Lakini ilipowajia haki kutoka kwetu, walisema: "Mbona hakupewa kama yale aliyopewa Musa (ya kugeuza fimbo nyoka na . . .)?" Je, hawakuyakataa yale aliyopewa Musa zamani, wakasema (juu yake na ndugu yake): "Ni wachawi wawili wanaosaidiana;" na wakasema: "Hakika sisi wote tunawakataa."

49. Sema: "Basi leteni Kitabu kitokacho kwa Mwenyezi Mungu ambacho kina uwongofu ulio bora kuliko hivi viwili (Taurati ya Nabii Musa na hii Qurani), ili nikifuata, kama nyinyi mnasema kweli."

50. Na kama hawakukujibu, basi juwa ya kuwa wanajifuatia tu matamanio yao. Na nani aliyepotea zaidi kuliko yule anayefuata matamanio yake pasi na uwongofu utokao kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhalimu (wa nafsi zao).

51. Na kwa yakini tuliwafululizia maneno (ya nasaha) ili wapate kukumbuka (Lakini wapi!)

52. Wale tuliowapa Kitabu kabla ya (hii Qurani) (baadhi) yao wanaiamini hii (Qurani).

53. Na wanaposomewa, husema: "Tunaiamini, bila shaka hii ni haki itokayo kwa Mola wetu; kwa yakini kabla ya haya tulikuwa wenye kujisalimisha (kwa Mwenyezi Mungu)."

54. Basi hao watapewa ujira wao mara mbili (kwa kumfuata Nabii Musa au Nabii Isa zamani, na sasa kumfuata Nabii Muhammad) na kwa kuwa walistahmili; na huondoa ubaya kwa wema, na hutoa (sadaka na zaka) katika yale tuliowapa.

وَمَا كُنْتَ ثَاوِيًا فِي أَهْلِ مَدْيَنَ تَتْلُو عَلَيْهِمْ
آيَاتِنَا وَلَكِنَّا كُنَّا مُرْسِلِينَ ۝

وَمَا كُنْتَ بِجَانِبِ الطُّورِ إِذْ نَادَيْنَا وَلَكِنْ رَحْمَةً
مِّنْ رَبِّكَ لِتُنْذِرَ قَوْمًا مَّا أَتَتْهُمْ مِّنْ نَّذِيرٍ مِّنْ
قَبْلِكَ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ۝

وَلَوْلَا أَن تُصِيبَهُمُ مُّصِيبَةٌ بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ
فَيَقُولُوا إِنَّا كُنَّا لَوَدَّا أَرْسَلَتْ إِلَيْنَا رَسُولًا قَدْ
آتَيْنَاكَ وَنَكُونُ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ۝

فَلَمَّا جَاءَهُمُ الْحَقُّ مِنْ عِنْدِنَا قَالُوا لَوْلَا أُوتِيَ
مِثْلَ مَا أُوتِيَ مُوسَىٰ أَوَّلَهُمْ يَكْفُرُوا بِمَا أُوتِيَ مُوسَىٰ
مِن قَبْلُ قَالُوا سِحْرَانِ تَظَاهَرَا وَقَالُوا إِنَّا بِكُمْ
كَافِرُونَ ۝

قُلْ فَأَنذَرْتُكُمْ يَوْمَ يَكُفُّ عَنِ اللَّهِ هُوَ أَهْدَىٰ مِنْهُمَا
أَتَّبِعُهُ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ۝

فَإِنْ لَّمْ يَتَّبِعُواكَ فَأَعْلَمَ أَنَّهُ يَتَّبِعُونَ أَهْوَاءَهُمْ
وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّنِ اتَّبَعَ هَوَاهُ بِغَيْرِ هُدًى مِّن
اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ۝

وَلَقَدْ وَصَّلْنَا لَهُمُ الْقَوْلَ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ۝

الَّذِينَ آمَنُوا مِنَّا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِهِ هُمْ بِهِ يُؤْمِنُونَ ۝

وَإِذَا يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ قَالُوا آمَنَّا بِهِ إِنَّهُ الْحَقُّ مِنْ
رَبِّنَا إِنَّا كُنَّا مِنْ قَبْلِهِ مُسْلِمِينَ ۝

أُولَٰئِكَ يُؤْتُونَ أَجْرَهُمْ مَّرَّتَيْنِ بِمَا صَبَرُوا وَيَدْرَءُونَ
بِالْحَسَنَةِ السَّيِّئَةَ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ ۝

55. Na wanaposikia upuzi hujitenga nao na husema (kuwaambia wapuzi hao): “Sisi tuna vitendo vyetu (vitakuwa malipo kwa ajili yetu) na nyinyi muna vitendo vyenu (vitakuwa malipo kwa ajili yenu); amani juu yenu (inayotokana na sisi — hamtasikia kwetu baya). Sisi hatutaki (kujibizana na) watu wajinga.”

56. Kwa hakika, wewe huwezi kumuongoa umpendaye, lakini Mwenyezi Mungu humuongoa amtakaye, Naye anawajua waongokao; (kwa hivyo anawaongoa na anawajua wasiotaka kuongoka, kwa hivyo anawaachilia mbali).

57. Na wakasema (makafiri wa Makka kumwambia Mtume): “Kama tukifuata uwongofu (huu uliokuja nao tukawa) pamoja nawe tutanyakuliwa kutoka nchi yetu (hii, yaani Waarabu watatupiga vita).” Je, hatukuwakalisha mahali patakatifu na pa amani, yanakovutiwa matunda ya kila aina (wakaletewa huko) kuwa riziki itokayo Kwetu? Lakini wengi wao hawajui (lolote, wanajisemea tu).

58. Na tumeiangamiza miji mingapi iliyojifaharisha juu ya maisha yao! Hayo, maskani yao yasiyokaliwa baada yao tena ila kidogo tu hivi; na sisi tumekuwa Warithi (wa hayo).

59. Na Mola wako haangamizi miji mpaka ampeleke Mtume katika mji wao mkuu, awesomee Aya zetu, (wakatae ndio waangamizwe,) wala hatuiangamizi miji mpaka watu wake wamekuwa madhalimu.

60. Na chochote mlichopewa, basi ni matumizi kwa maisha ya dunia na mapambo yake tu; lakini kilichoko kwa Mwenyezi Mungu ndicho bora na kitabaki; basi je, hamufahamu?

61. Je, mtu yule tuliyemuahidi ahadi nzuri — tena atakayoipata — atakuwa sawa na yule tuliyemnufaisha kwa manufaa ya maisha ya dunia tu, kisha siku ya Kiama awe miongoni mwa wataohudhurishwa (Motoni)?

62. Na (wakumbushe) siku atakapowaita (Mwenyezi Mungu) aseme: “Wako wapi washirika wangu ambao mlikuwa mkidai (kuwa washirika wangu).”

63. Watasema wale iliyothubutika juu yao kauli (ya adhabu ya Mwenyezi Mungu): “Mola wetu!

وَإِذَا سَمِعُوا اللَّغْوَ أَعْرَضُوا عَنْهُ وَقَالُوا لَنَا أَعْمَالُنَا وَلَكُمْ أَعْمَالُكُمْ سَلَامٌ عَلَيْكُمْ لَا تَبْتَغِ الْجَاهِلِينَ ﴿٥٥﴾

إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ ، وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ ﴿٥٦﴾

وَقَالُوا لَئِنْ تَتَّبِعِ الْهْدَىٰ مَعَكَ تَنُتْطِفَ مِنْ أََرْضِنَا أَوْ لَمْ تُكُنْ لَهُمْ حَرَمًا أَمِنًا يُجْبَىٰ إِلَيْهِ ثَمَرَاتُ كُلِّ شَيْءٍ رِزْقًا مِنْ لَدُنَّا وَلَكِنْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٥٧﴾

وَكَمْ أَهْلَكْنَا مِنْ قَبْلِكَ بَطَرْتَ مَعِيشَتَهَا، فَمَا لَكَ مَسْكِنُهُمْ لَمْ تُسْكَنْ مِنْ بَعْدِهِمْ إِلَّا قَلِيلًا، وَكُنَّا نَحْنُ الْوَارِثِينَ ﴿٥٨﴾

وَمَا كَانَ رَبُّكَ مُهْلِكَ الْقُرَىٰ حَتَّىٰ يَبْعَثَ فِي أُمَمٍ رَسُولًا يَنْتَلُوا عَلَيْهِمْ أَيْتِنَا، وَمَا كُنَّا مُهْلِكِي الْقُرَىٰ إِلَّا وَأَهْلُهَا ظَالِمُونَ ﴿٥٩﴾

وَمَا أَوْعَدْتُمْ مِنْ شَيْءٍ فَمَتَّاعِ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَزِينَتُهَا، وَمَا عِنْدَ اللَّهِ خَيْرٌ وَأَبْقَىٰ، أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٦٠﴾

أَفَمَنْ وَعَدْنَاهُ وَعَدًا حَسَنًا فَهُوَ لَا يَفِيهِ كَمَنْ مَتَّعْنَاهُ مَتَاعَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ثُمَّ هُوَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٦١﴾

وَيَوْمَ يُنَادِيهِمْ فَيَقُولُ أَيْنَ شُرَكَائِيَ الَّذِينَ كُنْتُمْ تَزْعُمُونَ ﴿٦٢﴾

قَالَ الَّذِينَ حَقَّ عَلَيْهِمُ الْقَوْلُ رَبَّنَا هَؤُلَاءِ

Hawa ndio tuliwapoteza; tuliwapoteza kama tulivyopotea; tunajiepusha nao mbele yako: hawakuwa wakituabudu sisi.”

64. Na itasemwa: “Waiteni washirika wenu.” Basi watawaita lakini hawatawajibu, na wataiona adhabu; laiti wanalikuwa wenye kuongoka (hapa ulimwenguni wakapata salama akhera).

65. Na (wakumbushe) siku atakayowaita Aseme: “Je, mliwajibu nini Mitume?”

66. Basi zitawapotea siku hiyo habari, nao hawataweza kuulizana.

67. Ama aliyetubia na akaamini na akafanya vitendo vizuri, asaa akawa miongoni mwa wenye kufuzu.

68. Na Mola wako huumba atakavyo na huchagua (atakavyo): Hawana (viumbe) hiari: Mwenyezi Mungu ameepekana na upungufu, na ametakasika na hao wawashirikishao (naye).

69. Na Mola wako anayajua yanayoficha vifua vyao na wanayoyadhihirisha.

70. Naye ndiye Mwenyezi Mungu, hakuna aabudiwaye kwa haki ila Yeye! Sifa zote njema — Mwanzoni na mwisho (duniapi na Akhera) — ni zake tu. Na hukumu pia ni yake, nanyi mtarudishwa kwake (kadhalika).

71. Sema: “Niambieni, kama Mwenyezi Mungu akiufanya usiku ukukalieni moja kwa moja mpaka siku ya Kiama, ni mungu gani asiyekuwa Mwenyezi Mungu atakayekuleteeni mwanga? Basi je, hamsikii?”

72. Sema: “Niambieni, kama Mwenyezi Mungu akiufanya mchana kukukalieni moja kwa moja mpaka siku ya Kiama, ni mungu gani asiyekuwa Mwenyezi Mungu atakayekuleteeni usiku, mnaopumua humo? Basi je, hamuoni (ihsani za Mwenyezi Mungu)?”

73. Na kwa rehema zake amekufanyieni usiku na mchana ili mpumue hapo usiku na mtafute fadhila zake (hapo mchana) na ili mpate kushukuru.

74. Na siku atakayowaita na kusema: “Wako wapi washirika wangu ambao mlikuwa mkidai (kuwa ni washirika wangu)?”

75. Na tutatoa katika kila uma shahidi (wao wa kuwashuhudia) tuwaambie ‘Leteni hoja zenu.’ Hapo watajua ya kwamba kweli iko kwa Mwenyezi Mungu na yatawapotea yale waliyokuwa wakiyazua.

الَّذِينَ آغْوَيْنَا أَغْوَيْنَاهُمْ كَمَا غَوَيْنَا تَبَرَّأْنَا إِلَيْكَ مَا كَانُوا إِيَّانَا يَعْبُدُونَ ۝

وَقَبِلْ أَدْعَا شُرَكَائِكُمْ فَمَا دَعَوْهُمْ فَلَمْ يَسْتَجِيبُوا لَهُمْ وَرَأَوُا الْعَذَابَ لَوْ أَنَّهُمْ كَانُوا يَهْتَدُونَ ۝

وَيَوْمَ يُنَادِيهِمْ فَيَقُولُ مَاذَا أَجَبْتُمُ الْمُرْسَلِينَ ۝ فَعِيتَ عَلَيْهِمْ أَلَّا يَكْفُؤَ يَوْمَئِذٍ قُلُوبُهُمْ لَا يَتَسَاءَلُونَ ۝

فَأَمَّا مَنْ تَابَ وَآمَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا فَغَسَّى ۝

وَرَبُّكَ يَخْلُقُ مَا يَشَاءُ وَيَخْتَارُ مَا كَانَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ سُبْحَانَ اللَّهِ وَتَعَالَى عَمَّا يُشْرِكُونَ ۝

وَرَبُّكَ يَعْلَمُ مَا تُكِنُّ صُدُورُهُمْ وَمَا يُعْلِنُونَ ۝

وَهُوَ اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ لَهُ الْحُجُودُ فِي الْأَوَّلِ وَالْآخِرَةِ رَوَاهُ الْحَكَمُ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ۝

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ جَعَلَ اللَّهُ عَلَيْكُمُ اللَّيْلَ سَرْمَدًا إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ مَنْ إِلَهٌ غَيْرُ اللَّهِ يَأْتِيكُمْ بِضِيَاءٍ أَوْ لَظْلَامٍ تَتَّبِعُونَ ۝

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ جَعَلَ اللَّهُ عَلَيْكُمُ النَّهَارَ سَرْمَدًا إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ مَنْ إِلَهٌ غَيْرُ اللَّهِ يَأْتِيكُمْ بِلَيْلٍ تَسْكُنُونَ فِيهِ أَوْ لَظْلَامٍ تُبْصِرُونَ ۝

وَمِنْ رَحْمَتِهِ جَعَلَ لَكُمْ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ لِتَسْكُنُوا فِيهِ وَلِتَبْتَغُوا مِنْ فَضْلِهِ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ۝

وَيَوْمَ يُنَادِيهِمْ فَيَقُولُ أَيْنَ شُرَكَائِيَ الَّذِينَ كُنْتُمْ تَزْعُمُونَ ۝

وَنَزَعْنَا مِنْ كُلِّ أُمَّةٍ شَهِيدًا فَقُلْنَا هَاتُوا بُرْهَانَكُمْ فَعَلِمُوا أَنَّ الْحَقَّ لِلَّهِ وَضَلَّ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَفْتَرُونَ ۝

76. Hakika Karuni alikuwa katika watu wa Musa, lakini aliwafanyia dhulma. Na tulimpa hazina ambazo funguo zake zinawatopeza watu wenye nguvu (kuzichukua). Walimwambia watu wake: “Usijione (usijigambe); hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wanaojiona.”

77. “Na utafute — kwa yale aliyokupa Mwenyezi Mungu — makazi mazuri ya akhera, wala usisahau sehemu yako ya dunia, na ufanye wema kama Mwenyezi Mungu alivyokufanyia, wala usitafute kufanya ufisadi katika nchi; bila shaka Mwenyezi Mungu hawapendi mafisadi.”

78. Akasema: “Hakika nimepewa haya kwa sababu ya ilimu niliyo nayo.” Je, hakujua ya kwamba Mwenyezi Mungu amewaangamiza kabla yake watu waliokuwa wenye nguvu zaidi kuliko yeye na wenye mkusanyo mwingi zaidi (kuliko wake yeye)? Na wabaya hawataulizwa makosa yao. (Mwenyezi Mungu mwenyewe anayajua yote).

79. Basi akawatokea watu wake katika pambo lake. Wakasema wale wanaotaka maisha ya dunia: “Laiti tungalipata kama aliyopewa Karuni; hakika yeye ni mwenye bahati kubwa.”

80. Na wakasema wale waliopewa ilimu: “Ole wenu! Malipo ya Mwenyezi Mungu ni mazuri kwa yule anayeamini na kufanya vitendo vizuri (kuliko aliyonayo huyu Karuni) wala hawatapewa hayo isipokuwa wafanyao subira.”

81. Basi tukamdidimiza yeye (Karuni) na nyumba yake ardhini; wala hapakuwa na kundi lolote la kumsaidia kinyume na Mwenyezi Mungu, wala hakuwa miongoni mwa walioweza kujisaidia.

82. Na wakawa wanasema wale waliotamani cheo chake jana: “E-e-e- (kweli) Mwenyezi Mungu humzidishia riziki amtakaye miongoni mwa waja wake (na hali ya kuwa mbaya, hampendi), Na hudhikisha (riziki ya anayemtaka); asingetufanyia hisani Mwenyezi Mungu bila shaka angetudidimiza (kama alivyomdidimiza kwani sisi tuliitamani hali yake) O! kweli hawafuzu makafiri.”

83. Hiyo nyumba ya akhera tutawafanyia wale wasiotaka kujitukuza katika ardhi wala (kufanya) ufisadi, na mwisho (mwema) utawathubutikia wacha-Mungu.

84. Atakayefanya wema atapata jaza bora kuliko huo (wema alioufanyia), na atakayefanya

إِنَّ قَارُونَ كَانَ مِنْ قَوْمِ مُوسَى فَبَغَى عَلَيْهِمْ وَآتَيْنَاهُ مِنَ الْكُنُوزِ مَا إِنَّ مَفَاتِحَهُ لَتَنُوءَ بِالْعُصْبَةِ أُولِي الْقُوَّةِ إِذْ قَالَ لَهُ قَوْمُهُ لَا تَفْرَحْ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْفَرِحِينَ ۖ

وَابْتَغِ فِيمَا آتَاكَ اللَّهُ الدَّارَ الْآخِرَةَ وَلَا تَنْسَ نَصِيبَكَ مِنَ الدُّنْيَا وَأَحْسِنْ كَمَا أَحْسَنَ اللَّهُ إِلَيْكَ وَلَا تَبْغِ الْفَسَادَ فِي الْأَرْضِ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْمُفْسِدِينَ ۖ

قَالَ إِنَّمَا أُوتِيتُهُ عَلَىٰ عِلْمٍ عِنْدِي ۚ أَوَلَمْ يَعْلَم أَنَّ اللَّهَ قَدْ أَهْلَكَ مِنْ قَبْلِهِ مِنَ الْقُرُونِ مَنْ هُوَ أَشَدُّ مِنْهُ قُوَّةً وَآكَثَرُ جَمْعًا وَلَا يُسْئَلُ عَنْ ذُنُوبِهِمُ الْمُجْرِمُونَ ۖ

فَخَرَجَ عَلَىٰ قَوْمِهِ فِي زِينَتِهِ ۚ قَالَ الَّذِينَ يُرِيدُونَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا لَبِيتَ لَنَا مِثْلَ مَا أُوتِيَ قَارُونَ ۚ إِنَّهُ لَكَا وَحِظٌ عَظِيمٌ ۖ

وَقَالَ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ وَيَلَكُمْ ثَوَابُ اللَّهِ خَيْرٌ لِمَنْ آمَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا وَلَا يُفْلِحُ إِلَّا الصَّابِرُونَ ۖ

فَخَسَفْنَا بِهِ وَبِدَارِهِ الْأَرْضَ ۖ فَمَا كَانَ لَهُ مِنْ فِئَةٍ يَنْصُرُوهُ مِنْ دُونِ اللَّهِ ۚ وَمَا كَانَ مِنَ الْمُنْتَصِرِينَ ۖ

وَاصْبِرْ الَّذِينَ تَحُمَلُونَ ۚ إِنَّهُمْ يَنْتَوُونَ عَنْ أَرْحَامِهِمْ يُقُولُونَ وَيَكُنَّا اللَّهُ يَبْطِ الرِّزْقَ لِمَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ وَيَقْدِرُ ۚ لَوْلَا أَنْ مَنَّ اللَّهُ عَلَيْنَا لَخَسَفَ بِنَاءُ وَيْكَانُهُ لَا يَفْلِحُ الْكَافِرُونَ ۖ

تِلْكَ الدَّارُ الْآخِرَةُ نَجْعَلُهَا لِلَّذِينَ لَا يُرِيدُونَ عُلُوًّا فِي الْأَرْضِ وَلَا فَسَادًا ۚ وَالْعَاقِبَةُ لِلْمُتَّقِينَ ۖ

مَنْ جَاءَ بِالْحَسَنَةِ فَلَهُ خَيْرٌ مِنْهَا ۚ وَمَنْ

ubaya, basi hawatalipwa wale wafanyao ubaya ila yale waliyokuwa wakiyafanya.

85. Hakika Yeye aliyekulazimisha (kufuata) Qurani, kwa yakini atakurudisha mahali pa kurejea! Sema: "Mola wangu ndiye amjuaye ajaye na uwongofu na yule aliyomo katika upotofu (upotevu) ulio dhahiri."

86. Nawe hukuwa unatumai ya kwamba utaletewa Kitabu (upate Utume); lakini ni rehema ya Mola wako; basi usiwe msaidizi wa makafiri.

87. Wala wasikuzuie kuzifuata Aya za Mwenyezi Mungu baada ya kufunuliwa kwako, na uwaite (watu) kwa Mola wako, wala usiwe miongoni mwa washirikina.

88. Wala usimuombe — pamoja na Mwenyezi Mungu — mungu mwingine; hakuna aabudiwaye kwa haki ila Yeye; kila kitu kitakufa isipokuwa Yeye (Mwenyezi Mungu basi). Hukumu (ya mambo yote) iko kwake, na kwake mtarejezwa (nyote).


جَاءَ بِالسَّبِيَّةِ فَلَا يُجْزَى الَّذِينَ عَمِلُوا السَّيِّئَاتِ
إِلَّا مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٨٥﴾

إِنَّ الَّذِينَ قُضِيَ عَلَيْكَ الْقُرْآنُ لَكُنْ لَهُ إِلَى
مَعَادٍ قُلُوبٌ رَئِيَّةٌ أَتَعْلَمُ مَنْ جَاءَ بِالْهُدَى
وَمَنْ هُوَ فِي ضَلَالٍ مُبِينٍ ﴿٨٦﴾

وَمَا كُنْتَ تَرْجُو أَنْ يُلْقَى إِلَيْكَ الْكِتَابُ إِلَّا
رَحْمَةً مِنْ رَبِّكَ فَلَا تَكُونَنَّ ظَهِيرًا لِلْكَافِرِينَ ﴿٨٧﴾

وَلَا يَصُدُّكَ عَنْ آيَاتِ اللَّهِ بَعْدَ إِذْ أَنْزَلَتْ
إِلَيْكَ وَادْعُ إِلَى رَبِّكَ وَلَا تَكُونَنَّ
مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿٨٨﴾

وَلَا تَدْعُ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ
كُلُّ شَيْءٍ هَالِكٌ إِلَّا وَجْهَهُ لَهُ الْحُكْمُ وَإِلَيْهِ
تَرْجَعُونَ ﴿٨٩﴾



SURATUL ANKABUUT

Ina Aya 69

(Imeteremka Makka)

Ina Makara 7

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuncemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuncemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Alif Lam Mym.

الْم ١

2. Je, watu wanadhani wataachwa (wasitiwe katika misukosuko) kwa kuwa wanasema "Tumeamini?" Basi ndio wasijaribiwe (wasipate mitihani)?

أَحْسِبَ النَّاسُ أَنْ يُتْرَكُوا أَنْ يَقُولُوا آمَنَّا وَهُمْ لَا يُفْتَنُونَ ٢

3. Hapana; bila shaka tuliwatia katika taabu wale waliokuwa kabla yao, na kwa yakini Mwenyezi Mungu atawatambulisha wale walio wa kweli na atawatambulisha (wale walio) waongo.

وَلَقَدْ فَتَنَّا الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ فَلَيَعْلَمَنَّ اللَّهُ الَّذِينَ صَدَقُوا وَلَيَعْلَمَنَّ الْكَاذِبِينَ ٣

4. Je, wanadhania wale wafanyao maovu kwamba watatushinda (tusiwapate kuwatia adhabu)? Hukumu mbaya hiyo wanayohukumu.

أَمْ حَسِبَ الَّذِينَ يَعْلَمُونَ السَّيِّئَاتِ أَنْ يَسْبِقُونَا سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ ٤

5. Mwenye kutaka kukutana na Mwenyezi Mungu, basi hakika ajali ya Mwenyezi Mungu itafika tu, (na asiyetaka kukutana na Mwenyezi Mungu pia ajali yake itamfikia). Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.

مَنْ كَانَ يَرْجُوا لِقَاءَ اللَّهِ فَإِنْ أَجَلَ اللَّهُ لَاحِقًا لَهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ٥

6. Na anayejitahidi, bila shaka anajitahidi kwa ajili (ya maslaha) ya nafsi yake; kwa hakika Mwenyezi Mungu si muhitaji wa walimwengu.

وَمَنْ جَاهَدَ فَإِنَّا يُجَاهِدُ لِنَفْسِهِ إِنَّ اللَّهَ لَغَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ ٦

7. Na walioamini na kufanya vitendo vizuri, kwa yakini tutawasamehe maovu yao, na tutawalipa mema ya yale waliyokuwa wakiyafanya.

وَالَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَنُكَفِّرَنَّ عَنْهُمْ سَيِّئَاتِهِمْ وَلَنَجْجزِيَنَّهُمْ أَحْسَنَ الَّذِي كَانُوا يَعْمَلُونَ ٧

8. Na tumemwusia mwanaadamu afanye wema kwa wazazi wake; na kama wakikushurutiza kunishirikisha na yale usiyo na ilimu nayo, basi usiwatii; kwangu ndiyo marejeo yenu, basi nitakwambieni mliyokuwa mkiyatenda.

وَوَصَّيْنَا الْإِنْسَانَ بِوَالِدَيْهِ حُسْنًا وَإِنْ جَاهَدَاكَ لِتُشْرِكَ بِي مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ فَلَا تُطِعْهُمَا إِلَىٰ مَرْجِعِكُمْ فَأُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ٨

9. Na walioamini na wakafanya vitendo vizuri bila shaka tutawatia katika watu wema.

وَالَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَنُدْخِلَنَّهُمْ فِي الصَّالِحِينَ ٩

10. Na katika watu wako wanaosema: "Tumemuamini Mwenyezi Mungu," lakini wanapoudhiwa katika (njia ya) Mwenyezi Mungu

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَقُولُ آمَنَّا بِاللَّهِ فَإِذَا أُوذِيَ فِي اللَّهِ

hufanya vile vituko vinavyowakuta kwa watu kama ni adhabu ya Mwenyezi Mungu. Na ikija nusura kutoka kwa Mola wako husema: "Bila shaka sisi tulikuwa pamoja nanyi." (Na hali ya kuwa ni waongo wanafiki). Je, Mwenyezi Mungu hajui yaliyomo vifuani mwa walimwengu?

11. Na hakika Mwenyezi Mungu atawabainisha wale walioamini, na atawatambulisha wanafiki.

12. Na waliokufuru walisema kuwaambia walioamini "Fuateni njia yetu sisi (Msimfuata Muhammad); nasi tutayabeba makosa yenu" (Iwe nyiye hapana la kukufikeni). Lakini hawataweza kubeba katika makosa yao chochote kile (iwe ndiyo basi kwa hao waliofanya makosa); hakika wao ni waongo tu.

13. Na hakika wataibeba mizigo yao, na mizigo mingine pamoja na mizigo yao (Nayo ni mizigo ya dhambi za kuwapoteza wenziwao, na hao wenye kupotezwa watachukua mizigo ya kukubali kufanya makosa). Na kwa vakini wataulizwa siku ya Kiama juu ya yale waliyokuwa wakiyazua.

14. Na bila shaka tulimtuma Nuhu kwa watu wake na akakaa nao myaka elfu kasoro myaka hamsini; (wasikubali kufuata), basi tufani iliwaifika (wakaghariki), na hali walikuwa madhalimu.

15. Na tukamuokoa yeye na watu wake (katika) safina, na tukaifanya (iwe) mazingatio kwa walimwengu.

16. Na (wakumbushe) Ibrahimu alipowaambia watu wake: "Muabuduni Mwenyezi Mungu na Mcheni: hayo ni heri kwenu; ikiwa mnajua (jambo jueni hili)."

17. "Hakika nyinyi mnayaabudu masanamu mkaacha (ibada ya) Mwenyezi Mungu, na mnatengenza uwongo; bila shaka wale mnaowaabudu mkamuacha Mwenyezi Mungu, wao hawakumilikiini riziki; takeni riziki kwa Mwenyezi Mungu, na Muabuduni na Mshukuruni. Kwake mtarudishwa, (siku ya Kiama).

18. Na kama mkikadhibisha, basi wamekwishakadhibisha watu wa kabla yenu (na wameangamizwa). Na si juu ya Mtume ila kufikisha waziwazi (ujumbe aliopewa)."

19. Je, hawaoni jinsi Mwenyezi Mungu aanzishavyo viumbe; kisha atavirudisha (mara ya pili) Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni sahali.

جَعَلَ فِتْنَةً لِلنَّاسِ كَعَذَابِ اللَّهِ وَلَئِنْ جَاءَ
نَصْرٌ مِّن رَّبِّكَ لَيَقُولُنَّ إِنَّا كُنَّا مَعَكُمْ أَوَلَيْسَ اللَّهُ
بَاعْلَمَ بِمَا فِي صُدُورِ الْعَالَمِينَ ⑩

وَلَيَعْلَمَنَّ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا وَلَيَعْلَمَنَّ الْمُنَافِقِينَ ⑪

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِلَّذِينَ آمَنُوا اتَّبِعُوا سَبِيلَنَا
وَلْنَحْمِلَ خَطِيئَتَكُمْ وَمَا هُمْ بِحَامِلِينَ مِنْ خَطِيئَتِهِمْ
مِّنْ شَيْءٍ إِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ ⑫

وَلَيَحْمِلُنَّ أَثْقَالَهُمْ وَأَنفَالًا مَّعَهُ أَثْقَالِهِمْ
وَلَيَسْأَلُنَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَمَّا كَانُوا يَفْعَلُونَ ⑬

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِهِ فَلَبِثَ فِيهِمْ
أَلْفَ سَنَةٍ إِلَّا خَمْسِينَ عَامًا فَأَخَذَهُمُ الطُّوفَانُ وَهُمْ
ظَالِمُونَ ⑭

فَأَنجَيْنَاهُ وَأَصْحَابَ السَّفِينَةِ وَجَعَلْنَاهَا آيَةً
لِّلْعَالَمِينَ ⑮

وَإِبْرَاهِيمَ إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاتَّقُوهُ ذَلِكُمْ
خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ⑯

إِنَّمَا تَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ أَوْثَانًا وَتَخْلُقُونَ
إِفْكًا إِنَّا لَنَعْلَمُ تَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ لَا
يَمْلِكُونَ لَكُمْ رِزْقًا فَاتَّبِعُوا عِندَ اللَّهِ الرِّزْقَ
وَاعْبُدُوهُ وَاشْكُرُوا لَهُ إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ⑰

وَإِنْ تَكْذِبُوا فَقَدْ كَذَّبَ أُمَمٌ مِّن قَبْلِكُمْ وَمَا عَلَى
الرَّسُولِ إِلَّا الْبَلَاغُ الْمُبِينُ ⑱

أَوَلَمْ يَرَوْا كَيْفَ يُبْدِئُ اللَّهُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ
إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ ⑲

20. Sema: "Tembeeni katika ardhi na tazameni jinsi alivyoanzisha kuumba, kisha Mwenyezi Mungu ndiye atakayeumba umbo la baadaye. Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.

21. Humuadhibu amtakaye (anapomuasi asitubie); na humrehemu amtakaye (anapofanya mema); na mtapelekwa kwake.

22. Na nyinyi hamuwezi kumshinda (Mwenyezi Mungu) ardhini wala mbinguni, nanyi hamuna mlinzi wala msaidizi kinyume cha Mwenyezi Mungu."

23. Na wale waliozikufuru Aya za Mwenyezi Mungu na kukutana naye, hao ndio watakata tamaa ya kupata rehema yangu, na hao ndio watakaopata adhabu iumizayo.

24. Basi haikuwa jawabu ya watu wake ila kusema: "Muueni au mtieni motoni, (mchomeni)." Basi Mwenyezi Mungu akamuokoa na Moto. Hakika muna katika haya mazingatio (makubwa) kwa watu wanaoamini.

25. Na alisema: "Hakika nyinyi mumefanya masanamu waola badala ya Mwenyezi Mungu. Na mnapendana baina yenu katika maisha ya dunia, lakini siku ya Kiama mtakataana wenyewe kwa wenyewe na mtalaaniana nyinyi kwa nyinyi, na makazi yenu yatakuwa Motoni; na hamtapata wa kukunusuruni."

26. Basi (Nabii) Luti akamuamini na akasema (Nabii Ibrahimu): "Hakika mimi nahamia katika (nchi aliyoniamrisha) Mola wangu, bila shaka yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima."

27. Na tulimpa (kumzaa Nabii) Is-haqa na (kumjuku Nabii) Yakubu, na tukauweka katika kizazi chake Unabii na (kupata) Kitabu, na tukampa ujira wake katika dunia; naye katika akhera kwa yakini atakuwa miongoni mwa watu wema.

28. Na (wakumbushe Nabii) Luti; alipowaambia watu wake: "Bila shaka nyinyi mnafanya uovu (ambao) hakuna yoyote aliyekutangulieni kwa (uovu) huo katika walimwengu."

28. Tumesema na kuandika mara nyingi ya kuwa hapana katika madhambi machafu yaliyokhusika na tupu mabaya zaidi kuliko haya ya wanaume kwa wanaume. Na jukumu kubwa zaidi sana analichukua huyo mfanyaji kuliko mfanyaji; na khasa zaidi kabisa akiwa anamuanzisha asiyepata kufanya. Na kwa kuanzishwa, basi na yeye ataendelea kufanya machafu hayo. Basi natutahadhari kweli kweli kufisidi watoto wa watu. Moja ya adabu atakazozipata ni kuona wake nao wanabaradhuliwa kama alivyowafanya mabaradhuli hao wa wengine. "Mla cha Mwenziwe na chake huliwa" na "Mosha Hoshwa" (Muosha huoshwa).

قُلْ سِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَانظُرُوا كَيْفَ بَدَأَ الْخَلْقَ
ثُمَّ اللَّهُ يُنشِئُ النَّشْأَةَ الْآخِرَةَ إِنَّ اللَّهَ عَلَى
كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ۝

يُعَذِّبُ مَنْ يَشَاءُ وَيَرْحَمُ مَنْ يَشَاءُ وَإِلَيْهِ
تُقْلَبُونَ ۝

وَمَا أَنْتُمْ بِمُعْجِزِينَ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ
وَمَا لَكُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ مِنْ وَلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ ۝

وَالَّذِينَ كَفَرُوا بِآيَاتِ اللَّهِ وَلِقَائِهِ أُولَئِكَ يَكُونُوا
مِنْ رَحْمَتِي وَأُولَئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ۝

فَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهِ إِلَّا أَنْ قَالُوا اقْتُلُوهُ أَوْ
حَرِّقُوهُ فَأَنجَاهُ اللَّهُ مِنَ النَّارِ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ
لِقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ۝

وَقَالَ إِنَّمَا اتَّخَذْتُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ أَوْثَانًا
مُودَّةَ بَيْنِكُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ثُمَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ
يَكْفُرُ بَعْضُكُم بِبَعْضٍ وَيَلْعَنُ بَعْضُكُم بَعْضًا
وَمَا أُولَئِكَ إِلَّا فِي شَرٍّ مِمَّا تَصِفُونَ ۝

فَأَمَنْ لَهُ لُوطٌ ۖ وَقَالَ إِنِّي مُهَاجِرٌ إِلَى رَبِّي
إِنَّهُ هُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ۝

وَوَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ وَجَعَلْنَا فِي ذُرِّيَّتِهِ
الْبِرَّ وَالْكِتَابَ وَآتَيْنَاهُ أَجْرَهُ فِي الدُّنْيَا
وَلَئِنَّ فِي الْآخِرَةِ لِمَنْ الصَّالِحِينَ ۝

وَلُوطًا إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ إِنَّكُمْ لَأَنْتَؤُنَ الْفَاحِشَةُ
مَا سَبَقَكُمْ بِهَا مِنْ أَحَدٍ مِنَ الْعَالَمِينَ ۝

29. "Je, mnawaendea wanaume, na mnawakatia njia (watu kwa kuwaua na kuwanyang'anya njiani) na mnafanya maovu katika mikusanyiko yenu?" Basi halikuwa jawabu ya watu wake ila kusema: "Tuletee adhabu ya Mwenyezi Mungu ikiwa umiongoni mwa wasemao kweli!"

30. Akasema: "Mola wangu! Ninusuru juu ya watu mafisadi (hawa)."

31. Na wajumbe wetu, (Malaika) walipomjia Ibrahimu na habari njema (ya kuwa atamzaa Nabii Is-haqa) walisema (vile vile) "Bila shaka tutawaangamiza watu wa mji huu, hakika watu wake wamekuwa madhalimu (wa nafsi zao)."

32. Akasema (Nabii Ibrahimu): "Hakika humo yumo Luti." Wakasema: "Sisi tunawajua sana waliomo humo, kwa yakini tutamuokoa yeye na watu wake ila mkewe aliye miongoni mwa watakaokaa nyuma."

33. Na wajumbe wetu walipomjia Luti, alihuzunika kwa ajili yao, na moyo wake uliona dhiki kwa ajili yao, basi (hao Malaika) walisema: "Usiogope wala usihuzunike, bila shaka sisi tutakuokoa wewe na watu wako ila mke wako aliye miongoni mwa watakaokaa nyuma."

34. "Kwa yakini sisi tutateremsha juu ya wenyeji wa nchi hii adhabu kutoka mbinguni kwa sababu ya kuasi (kwao)."

35. Na bila shaka tumeacha katika (nchi) hiyo Ishara wazi kwa watu wanaofahamu.

36. Na kwa Madiani (tulimtumia) ndugu yao, (Nabii) Shuebu, naye akasema: "Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu na iogopeni siku ya akhera wala msende katika ardhi mkifisidi."

37. Lakini walimkadhibisha, basi likawatoa roho tetemeko la nchi na wakawa ndani ya nyumba zao wenye kuanguka kifudifudi (wamekwishakufa).

38. Na pia Kina Adi na Thamudi (tuliwaangamiza). Na katika maskani yao kunakubainikieni (kuangamizwa kwao), na Shetani aliwapambia vitendo vyao (vibaya) na akawazuilia njia (za kheri) na hali ya kuwa walikuwa wenye kuona.

32. Mwema hawezi kuwaokowa vipenzi vyake Kiama wakiwa katika mabaya wamebobeza. Ametutajia Mwenyezi Mungu katika Aya ya 46 ya Surat Hud kutoweza Nabii Nuhu kumuokoa mwanawe aliyemtoa mgongoni mwake. Na akatuonyesha katika Aya ya 10 ya Suratut Tahrym kutoweza yeye wala Nabii Luti kuwaokoa wake zao. Na akatuonyesha katika Aya ya 114 ya Suratut Tawba kutoweza Nabii Ibrahimu kumuokoa Ami yake. Na katika Aya ya 56 ya Suratul Qasas kutoweza Mtume Muhammad s.a.w. kumuokoa kabisa kabisa Ami yake.

أَرْبَعَكُمْ لَتَأْتُنَّ الرِّجَالَ وَتَقْطَعُونَ السَّبِيلَ
وَتَأْتُونَ فِي نَادِيَكُمُ الْمُنْكَرَ فَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهِ إِلَّا أَنْ قَالُوا ائْتِنَا بِعَذَابِ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ الصَّادِقِينَ ①

قَالَ رَبِّ انصُرْنِي عَلَى الْقَوْمِ الْمُفْسِدِينَ ②
وَلَمَّا جَاءَتْ رُسُلُنَا إِبْرَاهِيمَ بِالْبُشْرَى قَالُوا إِنَّا مُهْلِكُوا أَهْلَ هَذِهِ الْقَرْيَةِ إِنَّ أَهْلَهَا كَانُوا ظَالِمِينَ ③

قَالَ إِنَّ فِيهَا لُوطًا قَالُوا نَحْنُ أَعْلَمُ بِمَنْ فِيهَا لَنَنْجِيَنَّهُ وَأَهْلَهُ إِلَّا امْرَأَتَهُ زَكَتْ مِنَ الْغَابِرِينَ ④

وَلَمَّا أَنْ جَاءَتْ رُسُلُنَا لُوطًا سِخَىٰ بِهِمْ وَضَاقَ بِهِمْ ذَرْعًا قَالُوا لَا تَخَفْ وَلَا تَحْزَنْ إِنَّا مُنْجِيُونَ
وَأَهْلَكَ إِلَّا امْرَأَتَكَ كَانَتْ مِنَ الْغَابِرِينَ ⑤

إِنَّا مُنْزِلُونَ عَلَىٰ أَهْلِ هَذِهِ الْقَرْيَةِ رِجْرًا مِنَ السَّمَاءِ بِمَا كَانُوا يَفْسُقُونَ ⑥

وَلَقَدْ تَرَكْنَا مِنْهَا آيَةً بَيِّنَةً لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ⑦

وَالِى مَدْيَنَ أَخَاهُمْ شُعَيْبًا فَقَالَ يَتَوَمَّرُ عِبَادُوا اللَّهَ وَارْجُوا الْيَوْمَ الْآخِرَ وَلَا تَتَّبِعُوا فِي الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ⑧

فَلَمَّا بَوَّاهُ فَأَخَذَتْهُمُ الرَّجْفَةُ فَأَصْبَحُوا فِي دَارِهِمْ جِثِيمِينَ ⑨

وَعَادًا وَثَمُودًا وَقَدْ رَبَّيْنَاهُمْ كَمَا كُنْتُمْ تُسْكِنُهُمْ وَزَيْنًا لَهُمُ الشَّيْطَانُ أَغْمَا لَهُمْ فُصْلًا عَنْ السَّبِيلِ وَكَانُوا مُصْتَبِرِينَ ⑩

39. Na (vile vile) Karuni na Firauni na Hamana (waliangamizwa); na hakika aliwajia Musa kwa miujiza waziwazi, lakini walijivuna katika ardhi, lakini hawakuweza kumshinda (Mwenyezi Mungu).

40. Basi kila mmoja tulimtesa kwa sababu ya dhambi zake; miongoni mwao wako tuliowapelekea kimbunga cha changarawe; na miongoni mwao wako waliotolewa roho kwa ukelele mkubwa (uliopigwa na Jibrili); na miongoni mwao wako tuliowadidimiza ardhini; na miongoni mwao wako tuliowagharikisha. Na hakuwa Mwenyezi Mungu Mwenye kuwadhulumu, lakini walikuwa wakijidhulumu (wenyewe) nafsi zao.

41. Mfano wa wale waliofanya waungu asiyekuwa Mwenyezi Mungu, ni kama mfano wa buibui ajitandiaye nyumba (yake ili imhifadhi, nayo haimhifadhi na lolote); na bila shaka nyumba iliyo dhaifu kuliko zote ni nyumba ya buibui; laiti wanalijua!

42. Kwa yakini Mwenyezi Mungu anajua huko kuabudu kwao vyengine wakamuacha yeye (Mwenyezi Mungu); naye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima.

43. Na hiyo mifano tunawapigia watu; na hawaifahamu ila wajuao.

44. Mwenyezi Mungu ameziumba mbingu na ardhi kwa haki. Kwa hakika katika hayo zimo hoja (dhahiri) kwa wanaoamini.

45. Soma ulioletewa Wahyi (uliyofunuliwa) katika Kitabu (hiki ulicholetewa) na usimamishe Sala. Bila shaka Sala (ikisaliwa vilivyo) humzuiliya (huyo mwenye kusali na) mambo machafu na maovu, na kwa yakini kumbuko la Mwenyezi

وَقَارُونَ وَفِرْعَوْنَ وَهَامَانَ وَقَدْ
جَاءَهُمْ مُوسَى بِالْبَيِّنَاتِ فَاسْتَكْبَرُوا
فِي الْأَرْضِ وَمَا كَانُوا لَاسِقِينَ ﴿٣٩﴾

فَكُلًّا أَخَذْنَا بِذُنُوبِهِمْ فَمِنْهُمْ مَنْ أَرْسَلْنَا عَلَيْهِ
حَاصِبًا وَمِنْهُمْ مَنْ أَخَذَتْهُ الطَّيْفَةُ وَمِنْهُمْ مَنْ
خَسَفْنَا بِهِ الْأَرْضَ وَمِنْهُمْ مَنْ أَغْرَقْنَا وَمَا
كَانَ اللَّهُ لِيُظْلِمَهُمْ وَلَكِنْ كَانُوا أَنْفُسَهُمْ
يُظْلِمُونَ ﴿٤٠﴾

مَثَلُ الَّذِينَ اتَّخَذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ أَوْلِيَاءَ
كَثَلِ الْعَنْكَبُوتِ إِذَا أَخَذَتْ بَيْتًا ۖ وَإِنَّ أَوْهَنَ
الْبُيُوتِ لَبَيْتُ الْعَنْكَبُوتِ لَكَوْكَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿٤١﴾
إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا يُدْعُونَ مِنْ دُونِهِ مِنْ
شَيْءٍ ۚ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٤٢﴾

وَتِلْكَ الْأَمْثَالُ لَضَرِبُهَا لِلنَّاسِ وَمَا يَعْقِلُهَا
إِلَّا الْعَالِمُونَ ﴿٤٣﴾

خَلَقَ اللَّهُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ ۚ
إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِلْمُؤْمِنِينَ ﴿٤٤﴾

أَتْلُ مَا أُوْحِيَ إِلَيْكَ مِنَ الْكِتَابِ وَأَقِمِ الصَّلَاةَ ۚ
إِنَّ الصَّلَاةَ تَنْهَى عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ ۚ وَلَذِكْرُ اللَّهِ

41. Hapa ni kama vile tunavyosema kila siku kuwa wa kuombwa akaweza (a) kuondoa mabaya, au (b) kuleta mema ni Mwenyezi Mungu tu peke yake si Sharifu wa Mtaa wa Mackinon Road wala Sharifu wa mtaa wa Sharifu Musa wala Shekhe wa mtaa wa Mtoni wala Shekhe wa mtaa wa Fujoni, wala mzimu wa Baa Farjallah wala pepo wa Vura wala wengineo wala mengineyo.

Mambo yote ni ya Mungu
Ndiye Pweke Mwenye Quwa

Atakalo ndilo huwa
Mwenye amri na shani.

43. Hapa Aya hii — kama Aya ya 22 ya *Suratur Rum* na ya 15 ya *Suratul Ankabuut* na nyinginezo — inahimiza kusoma kwani kwa kusoma ndipo utapofahamu hayo ambayo Mwenyezi Mungu na Mitumewe wanayasema. Na kuyajua hayo na kuyafwata ndio kutengenekeza duniani na akhera.

45. Baadhi ya wakubwa wa Dhikiri wanaotaka kupoteza watu wanalifasiri vibaya — makusudi — hili tamko la *Waladhikrullahi Akbar*. Wanasema dhikiri ndiyo bora kuliko Sala. Khiari yao. Watachukua mizigo yao na mizigo ya hao wawapoteza. Katika Uislamu — baada ya mtu kuwa Mwislamu — hapana amali bora kuliko Sala na ndiyo farka baina ya Uislamu na ukafiri. Basi, khiari yao; nawapoteze watu.